BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo-TAZARA, S.L.P. 76068,
15471 DAR ES SALAAM, Tanzania.
Barua pepe: info@heslb.go.tz; **Tovuti**: www.heslb.go.tz

MWONGOZO WA UTOAJI MIKOPO NA RUZUKU KWA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021

1.0 MAELEKEZO MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE WAOMBAJI MIKOPO

Waombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo **2020/2021** wanafahamishwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(i) Kusoma na kufuata taratibu za maombi katika Mwongozo huu wa mwaka wa masomo **2020/2021;**

(ii) Kuhakikisha kuwa namba ya mtihani wa kidato cha nne iwe sawa kwenye maombi ya mkopo na udahili wa chuo;

(iii) Waombaji ambao wamefanya mitihani ya kidato cha nne zaidi ya mara moja wahakikishe wanaorodhesha namba zote katika maombi yao;

(iv) Kuhakikisha kuwa nyaraka zote za maombi ya mkopo unazowasilisha ziwe zimehakikiwa na mamlaka husika;

(v) Kuhakikisha kwamba vyeti vyote vya kuzaliwa/vifo vinathibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini **(RITA)** au wakala Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar au Afisa aliyeteuliwa ili kuthibitisha uhalali huo;

(vi) Kuhakikisha vyeti vyote vya kuzaliwa/vifo kwa Wanafunzi waliozaliwa nje ya nchi au wazazi waliofariki nje ya nchi vithibitishwe na ofisi za ubalozi husika zilizopo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vii) Waombaji wajaze fomu zao kwa usahihi kabla ya kuziwasilisha;

(viii) Maombi ya mikopo yanapaswa kuwa na taarifa sahihi na za kweli;

(ix) Waombaji wote wanatakiwa kutunza nakala ya fomu ya maombi ya mkopo waliyowasilisha Bodi ya Mikopo kwa matumizi mengine (kama itahitajika);

(x) Waombaji wote wanakumbushwa kuzingatia muda wa mwisho wa kutuma maombi ambao ni **Jumatatu, Agosti 31, 2020.**

2.0 KWA UFUPI

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilianzishwa mwaka 2004 kupitia Sheria ya HESLB **(SURA 178)** na kuanza kazi rasmi **Julai, 2005**. Bodi ya Mikopo ina majukumu makuu mawili ambayo ni kutoa mikopo au ruzuku kwa wanafunzi wahitaji waliokidhi vigezo.

3.0 USTAHIKI

Sheria na kanuni za Bodi ya Mikopo zimeainisha sifa na vigezo vya jumla kwa wanafunzi wahitaji wa mikopo. Mwombaji **stahiki** na **mhitaji** anaweza kuomba mkopo /ruzuku ili kugharamia gharama za masomo ya elimu ya juu.

3.1 Mwombaji mhitaji

Mbali na sifa za jumla, vigezo vya ziada vinafafanua mwanafunzi mhitaji asizidi umri wa **miaka 35** katika kipindi anachoomba mkopo, ambaye ni:

(i) Yatima (ambaye amepoteza wazazi wote wawili) au aliyepoteza mzazi mmoja, awasilishe cheti cha kifo kilichothibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini **(RITA)** au
Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar **(ZCSRA);**

(ii) Mwombaji mwenye ulemavu uliothibitishwa na Mganga Mkuu wa Mkoa (**RMO),** au Wilaya (**DMO),** au chombo chochote kilichoidhinishwa kuthibitisha hali hiyo.

(iii) Mzazi mwenye ulemavu uliothibitishwa na Mganga Mkuu wa Mkoa (**RMO),** au Wilaya (**DMO),** au chombo chochote kilichoidhinishwa kuthibitisha hali hiyo.

(iv) Mwombaji anayetoka kwenye familia ya kipato cha chini au kaya maskini ambapo elimu ya sekondari au stashahada (diploma) alifadhiliwa na taasisi inayotambulika. Waombaji wa aina hii wanatakiwa kupakua fomu kutoka katika tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz) ambayo itajazwa na mfadhili na iambatishwe na nyaraka nyingine katika mtandao.

(v) Mwombaji anayetoka kwenye familia ya kipato cha chini au kaya maskini inayohudumiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) anatakiwa kuambatanisha namba ya TASAF uhitaji wake.

3.2 Sifa za Jumla ambazo zinatambulika kisheria

Vigezo vya jumla vinamtaka mwombaji mkopo atimize masharti yafuatayo: -

(i) Awe Mtanzania;

(ii) Awe ameomba mkopo kupitia mfumo wa maombi ya mkopo (OLAMS);

(iii) Awe amedahiliwa katika taasisi ya elimu ya juu yenye ithibati, kwa muda wote (full time) isipokuwa wanafunzi wanaodahiliwa kusoma katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Open University of Tanzania);

(iv) Asiwe na ufadhili mwingine kwa masomo yake ya elimu ya juu;

(v) Mwanafunzi anayeendelea na masomo anayeomba mkopo mwenye matokeo/ripoti za matokeo zinazoonesha ufaulu wa masomo yake ili kumwezesha kuendelea na masomo mwaka unaofuata au kwenda hatua nyingine ya masomo;

(vi) Kwa mwanafunzi mnufaika ambaye anataka kuomba tena mkopo baada ya kusitisha masomo/chuo anatakiwa alipe angalau **asilimia 25** ya fedha aliyoitumia kabla

hajaomba mkopo mpya. Malipo ya **25%** ya mkopo wa awali siyo dhamana ya kupangiwa mkopo;

3.3 Vigezo na stahiki nyingine

(i) Mkopo utatolewa kwa kuzingatia **uhitaji na programu;**

(ii) Waombaji wapya ambao kwa sasa wanaendelea na masomo, lazima wawe wamehitimu elimu ya kidato cha sita (**ACSEE)** au stashahada (diploma) ndani ya **miaka mitano,** kuanzia mwaka **2016** hadi **2020**.

(iii) Waombaji wote waliodahiliwa kusoma shahada mbalimbali kwa mwaka wa masomo **2020/2021** wanapaswa wawe wame**hitimu kidato cha sita/Stashahada** au sifa nyingine linganishi katika kipindi cha miaka mitano, yaani kati ya **2016 na 2020**.

4.0 MAKUNDI YA PROGRAMU

Baada ya kuainisha waombaji wahitaji na kuonesha taratibu katika kipengele 3.1 na 3.2 hapo juu, makundi ya programu zifuatazo zenye vipaumbele zitapewa mikopo kulingana na uwepo wa fedha.

4.1 Kundi la Kwanza

Kozi katika kundi la kwanza ni: -

(i) **Ualimu wa Sayansi** (Fizikia, Kemia na Baiolojia) na Ualimu wa Hisabati;

(ii) **Sayansi za Afya** (Udaktari, Upasuaji Meno, Madawa ya Mifugo, Ufamasia, Uuguzi, Ukunga, Shahada ya Sayansi katika Prosthetikia na Mifupa, Shahada ya Sayansi katika Mazoezi ya Viungo, Shahada ya Sayansi ya Afya na Maabara, Shahada ya Sayansi ya Maabara na Matibabu na Shahada ya Sayansi ya Teknolojia ya Mionzi;

(iii) **Programu za Uhandisi** (Ujenzi, Mitambo, Umeme, Uchimbaji Madini, Utengenezaji Nguo, Kemikali na Usindikaji, Kilimo, Chakula na Usindikaji, Magari, Viwanda, Usafiri Majini, Teknolojia ya Uhandisi wa Baharini, Elektronikia na Mawasiliano, Kompyuta, Programu za Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mitandao, Mazingira, na Mipango Miji, Usindikaji na Huduma baada Mavuno, Maji na Umwagiliaji, Petroli na Gesi, Umeme na Shahada ya Uhandisi wa Maabara; Uhandisi wa Ndege; na Uhandisi wa Maabara za Afya;

(iv) Jiolojia ya Petroli, Kemia ya Petroli;

(v) Kilimo, Misitu, Sayansi ya Wanyama na Uzalishaji.

4.2 Kundi la Pili

Kozi katika kundi hili ni:

(i) **Programu za Msingi za Sayansi** (Shahada ya Sayansi kwa ujumla katika Wanyama, Mimea, Kemia, Fizikia, Baiolojia, Baiolojia ya Viumbe Vidogo, Baiolojia ya Mifugo na Bioteknolojia, Uvuvi na Mifugo, Sayansi ya Mazingira na Uhifadhi, Matibabu, Hisabati na Takwimu, Sayansi ya Mazingira na Usimamizi, Afya na Mazingira, Baioteknolojia na Maabara, Wanyamapori na Uhifadhi, na Kompyuta); TEHAMA, Vipimo na Mizani, Mazingira na Maendeleo ya Miji.

Programu ya Sayansi ya Ardhi (Ubunifu Majengo, Ubunifu Mandhari nje ya Majengo, Usanifu ndani ya Majengo, Uchumi Ujenzi, Mipango Miji na Vijiji, Usimamizi na Uthaminishi Ardhi, Jiospasho, Teknolojia katika Usanifu).

4.3 Kundi la Tatu

(i) Programu katika kundi hili ni pamoja na Masomo ya Biashara na Uongozi, Sayansi za Jamii, Sanaa, Sheria, Lugha, Fasihi na Masomo ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano.
(ii) Programu nyingine zote ambazo hazijaorodheshwa katika kundi lolote kati ya hayo matatu, zitaangukia katika kundi la tatu.

5.0 VIPENGELE VYA MIKOPO, KING'AMUA UWEZO NA FEDHA INAYOPANGWA

Kwa kuzingatia uhitaji na matokeo ya kinga'amuzi uwezo Bodi ya Mikopo

inaweza kulipia gharama za baadhi au vipengele vyote hapo chini:

(i) Gharama za Chakula na Malazi
(ii) Ada ya Mafunzo
(iii) Vitabu na Viandikwa
(iv) Mahitaji Maalum ya Kitivo
(v) Utafiti
(vi) Mafunzo kwa Vitendo

5.1 Kipima/king'amua Uwezo

Kipima uwezo kitatumika kuonesha uhitaji wa kifedha wa mwombaji. Malipo ya ada iliyolipwa shule za sekondari (CSEE, ACSEE) pamoja na Stashahada (diploma) ni kigezo kimojawapo kinachoangaliwa kubaini uwezo wa kuchangia gharama za elimu ya juu, vingine ni uyatima, ulemavu, ufadhili na familia maskini.

Kwa maana hiyo, uhitaji utapimwa tofauti kati ya gharama za mwaka katika programu ya elimu ya juu katika taasisi husika ya elimu ya juu dhidi ya gharama iliyotumika kulipia elimu ya sekondari au stashahada (diploma) na uwezo wa mwombaji alioubainisha katika elimu ya sekondari au diploma kama ishara ya uwezo wa mwombaji kuchangia gharama za elimu ya juu.

5.2 Mgawanyo wa fedha katika vipengele vya mikopo

Upangaji mikopo kwa waombaji waliofanikiwa kupata mikopo utagawanywa kwa kuanza na gharama za chakula na malazi, ikifuatiwa na Ada ya mafunzo, kisha vitabu na viandikwa vikifuatiwa na mahitaji maalum ya kitivo, utafiti, na mwisho mafunzo kwa vitendo, kulingana na kiasi cha fedha kilichobakia kutoka vipengele vilivyotangulia.

5.3 Kiwango cha Ada ya Mafunzo

Kiwango cha juu cha ada ya mafunzo kwa waombaji wote watakaofanikiwa kupata mikopo kitakuwa sawa na gharama za ada ya mafunzo zilizoidhinishwa kwa mwaka huu zinazolipwa katika vyuo vikuu vya umma.

5.4 Mwanafunzi anayeendelea na masomo na ambaye ni Mnufaika wa Mkopo

Kwa wanafunzi wote wanufaika wa mikopo wanaoendelea na masomo wataendelea kupokea mikopo kama awali kulingana na ufaulu wa mitihani yao. Wanafunzi wanaoendelea na masomo ambao ni wanufaika wa mikopo HAWAHITAJIKI KUOMBA TENA MKOPO.

5.5 Utaratibu wa Malipo: Gharama za chakula na malazi, vitabu na viandikwa, mafunzo kwa vitendo, gharama za tafiti *yatalipwa moja kwa moja kwa mwanafunzi* wakati Ada ya mafunzo na mahitaji maalum ya kitivo yatalipwa moja kwa moja kwenye taasisi husika ya elimu ya juu.

6.0 WAOMBAJI WA MIKOPO NJE YA NCHI (SHAHADA ZA KWANZA NA ZA UZAMILI)

Wanafunzi stahiki wa mikopo kwa mwaka wa masomo **2020/2021** waliodahiliwa kusoma katika vyuo vya nje ya nchi wanapaswa kutimiza masharti yaliyoorodheshwa katika Vigezo vya Jumla Sehemu ya 3.2.

Pamoja na vigezo na masharti yaliyotajwa katika Sehemu ya 3.2, waombaji wa mikopo waliochaguliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pekee ndio watakaokuwa na sifa za kupatiwa mikopo ya fedha za kujikimu isiyozidi **Dola za Kimarekani 5,400** kwa mwaka. Wanafunzi husika wanapaswa kuchaguliwa kusoma nje ya nchi katika nchi ambazo zina makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7.0 MASHARTI MENGINE KATIKA UTOAJI MIKOPO

7.1 Wajibu wa Wadhamini na Wazazi

Wazazi na wadhamini wana wajibu wa kuthibitisha usahihi wa taarifa waombaji zao binafsi ambazo zimewasilishwa katika fomu ya maombi ya mkopo kabla ya kusaini. Wadhamini wanatakiwa kuhakikisha mikopo inarejeshwa na wanapaswa kufahamu mahali wakopaji walipo na ikitokea mnufaika hajamaliza kulipa, ***mdhamini atalazimika kulipa mkopo huo*.**

Mdhamini anatakiwa kutumia nakala ya kitambulisho kimojawapo kati ya hivi ambayo imethibitishwa na hakimu au wakili:

i. Kitambulisho cha Taifa
ii. Kadi ya mpiga kura
iii. Leseni ya udereva
iv. Pasi ya kusafiria
v. Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

7.2 Urejeshaji Mikopo

Baada ya kuhitimu au kusitisha masomo ya elimu ya juu, mnufaika wa mkopo atatakiwa kurejesha mkopo kwa makato si chini ya asilimia kumi na tano (15%) ya mshahatra wake wa kila mwezi. Mnufaika ambaye amejiajiri anapaswa kurejesha mkopo wake kwa kiwango kisichopungua shilingi laki moja (100,000/=) kwa mwezi au 10% ya pato lake linalotozwa kodi.

7.2.1 Ada na Tozo za Urejeshaji Mikopo

7.2.1.1 Tozo ya Kulinda Thamani ya Fedha (Value Retention Fee)

Ili kuhakikisha mfuko wa ukopeshaji unakuwa endelevu, Tozo ya Kulinda Thamani ya Fedha itakatwa asilimia sita (6%) kwa mwaka tangu tarehe mnufaika alipohitimu masomo yake.

7.2.1.2 Ada ya Uendeshaji (Loan Administration Fee)

Bodi ya Mikopo itakata asilimia moja (1%) ya ada ya uendeshaji kwenye mkopo halisi wa mnufaika. Ada hii itakatwa mara moja tu.

7.2.1.3 Ada ya Makato ya Adhabu (Penalty)

Ikiwa mnufaika atashindwa kulipa mkopo baada ya kipindi cha matazamio (grace period) cha miezi 24 baada ya kuhitimu masomo yake, atatozwa adhabu ya asilimia kumi (10%) ya mkopo wote.

8.0 KUHAMA CHUO AU PROGRAMU NDANI YA CHUO

HESLB haitafanya malipo ya mkopo kwa wanafunzi ambao watahama vyuo kwa hiari yao wenyewe. Baada ya kupokea uthibitisho wa uhamisho wa mwanafunzi kutoka kwa mamlaka husika, uhamisho wa mkopo utafanyika. Hakuna uhamisho wa mkopo utakaofanyika zaidi ya siku mia moja ishirini (120) baada ya kutangazwa taarifa za udahili. **Uhamisho wa mkopo utafanyika kulingana na kiasi cha mkopo kilichopangwa awali.**

Orodha ya Waombaji waliopangiwa kwenye Taasisi za Elimu ya Juu
HESLB itazingatia maombi ya mkopo kutoka kwa wanafunzi waliodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu na kuthibitishwa na kuwasilishwa HESLB na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) au mamlaka nyingine iliyothibitishwa.

9.0 JINSI YA KUOMBA MKOPO

Maombi yote ya mkopo yatafanyika kupitia Mfumo wa Maombi na Usimamizi wa Mikopo (OLAMS). Waombaji wote wa mikopo **WANAKUMBUSHWA** kutumia namba ileile ya Mtihani wa Kidato cha Nne iliyotumika wakati wanapoomba udahili vyuo.

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa maombi kwenye mtandao, waombaji watapaswa kutoa nakala za fomu za mombi na mikataba ya mkopo kwenye mtandao, kugonga mihuri sehemu husika, kusaini fomu, kuambatanisha nyaraka zinazohitajika kwenye mtandao wa OLAMS kabla ya kutuma maombi hayo kwa njia ya EMS kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo,
Eneo la TAZARA,
S.L.P 76068,
15471 Dar es salaam, TANZANIA.

Waombaji wanakumbushwa kutunza nakala ya fomu za maombi, viambatanisho vilivyowasilishwa na risiti ya EMS iliyotumiwa kutuma maombi yao kwa kufuatilia HESLB endapo itahitajika.

10.0 Ada ya Maombi ya Mkopo

Waombaji wanapaswa kulipia ada ya maombi ya mkopo ya kiasi cha shilingi elfu thelathini (30,000) kupitia Benki ya NMB, CRDB au TPB au kwa mitandao ya simu ya M-PESA, TIGO PESA, na AIRTEL MONEY. Kwa maelezo zaidi tembelea: **https:/olas.heslb.go.tz**

10.1 Mwisho wa Kupokea Maombi

Dirisha la maombi ya Mkopo kwa mwaka **2020/2021** litafunguliwa kuanzia tarehe **21 Julai, 2020 hadi tarehe 31 Agosti, 2020.**

Orodha ya Waombaji Watakaopangiwa Mikopo

Orodha ya waombaji watakaofanikiwa kupangiwa mikopo itatangazwa kwenye tovuti ya HESLB:
www.heslb.go.tz na kwenye akauti za kudumu za waombaji mikopo SIPA kabla au tarehe 10 Novemba, 2020.

11.0 Kukata Rufaa

Waombaji ambao hawataridhika na viwango vya mikopo watakayopangiwa wanaweza kukata rufaa kwa kukamilisha fomu za rufaa kwenye mtandao (OLAMS). Maelezo zaidi yatatolewa baadaye.

12.0 Maulizo na Malalamiko

Waombaji au wanufaika wa mikopo wenye maswali au malalamiko watapaswa kufuata taratibu zilizotolewa kwenye dirisha la maombi ya mkopo.

13.0 Wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu

Wanafunzi watakaokopeshwa kwa mwaka wa masomo **2020/2021**, waliodahiliwa kujiunga na Shahada za Uzamili na Uzamivu wanapaswa kuwa na sifa za jumla zilizoorodheshwa katika kipengele cha 3.2 hapo juu.

13.1 Wanafunzi wa Uzamili na Uzamivu (Wahadhiri)

Mbali na sifa za jumla, waombaji wa Shahada za Uzamili na Uzamivu lazima wawe na vigezo maalum vya kundi hilo, ambavyo ni:

(i) Wanapaswa wawe na Shahada ya Kwanza au Stashahada ya Juu na kiwango cha chini cha ufaulu kiwe ni Daraja la Pili la Juu (Kwa waombaji wa Shahada ya Uzamili) au Shahada ya Uzamili na kiwango cha chini cha ufaulu kiwe Daraja la Pili la Juu (Kwa waombaji wa Shahada ya Uzamivu).

(ii) Wanapaswa kuwa wahadhiri wa taasisi za elimu ya juu watakaodahiliwa kusoma masomo yao katika taasisi za elimu ya juu zinazotambulika nchini Tanzania.

(iii) Wanapaswa kuteuliwa na kupatiwa kibali kutoka kwa mwajiri ambaye ni Mkuu wa Chuo wa taasisi husika.

(iv) Wanapaswa kuwa wameanza kurejesha mikopo yao ya awali angalau kwa muda usiopungua miezi kumi na miwili (12) au kurejesha kwa mkupuo mkopo stahiki kwa waombaji ambao awali walinufaika na mikopo ya wanafunzi.

(v) Mwajiri lazima awe amesaini mkataba kati ya HESLB na taasisi husika ya elimu ya juu.

13.2 Wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu kwenye Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST)

Ili kuimarisha uwezo wa taifa katika utafiti, TEHAMA na uvumbuzi, HESLB inatoa mikopo kwa wanafunzi waliodahiliwa kusoma Shahada za Uzamili na Uzamivu katika masomo yanayohusiana na Sayansi katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST). Wanafunzi watakaokopeshwa kwa mwaka wa masomo 2020/2021, wanapaswa kuwa na sifa za jumla zilizoainishwa katika kipengele cha 3.2 hapo juu.

Mbali na sifa za jumla zilizoainishwa katika kipengele 3.2 hapo juu, waombaji wa Uzamili NM-
AIST lazima watimize vigezo vingine maalum kwa Wanafunzi wa taasisi hiyo:

(i) Wawe wamedahiliwa katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) katika shahada ya Uzamili au Shahada ya Uzamivu katika mojawapo ya kozi za kipaumbele hapo chini:

- Sayansi ya Maisha
- Uhandisi wa Sayansi ya Hisabati na Kompyuta.
- Uhandisi wa Sayansi ya Habari na Mawasiliano.
- Sayansi ya Vifaa, Nishati, Maji na Mazingira.

(ii) Lazima wawe ni waajiriwa katika Taasisi za Umma na wawe wamefanya kazi kwa muda usiopungua miaka miwili (2).

(iii) Lazima wawe wamedhaminiwa na waajiri wao kuhusiana na urejeshaji wa mikopo hiyo.

(iv) Lazima wawe wameanza kurejesha mikopo ya awali angalau kwa muda usiopungua miezi kumi na mbili au kwa mkupuo kwa jumla ya miezi kumi na mbili kama hapo awali walikuwa wanufaika wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

(v) Marejesho ya mikopo ya wanafunzi wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu wa NM-AIST yataanza mara tu baada ya kumaliza mwaka wa kwanza wa masomo, kwa

mwajiri kuwasilisha Bodi ya Mikopo makato ya kila mwezi kutoka kwenye mshahara wa mnufaika.

13.3 Wanafunzi wa Stashahada ya Uzamili waliodahiliwa katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LASCOT)

Wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (Law School of Tanzania) wanaostahili kukopeshwa kwa mwaka wa masomo **2020/2021** lazima wawe wametimiza masharti yafuatayo:

Lazima wawe na sifa za jumla zilizowekwa kipengele cha **3.2** hapo juu.

Mbali na sifa za jumla zilizowekwa kipengele cha **3.2** hapo juu, waombaji wa mikopo katika Shule ya Sheria Tanzania (LASCOT) lazima wawe na vigezo maalum, ambavyo ni: -

(i) Wawe wamehitimu Shahada ya Sheria si zaidi ya miaka mitano nyuma **(2016 hadi 2020);**

(ii) Mikopo itatolewa kwa waombaji wahitaji tu kulingana na matokeo ya king'amua uwezo wa mwombaji.

(iii) Ikiwa mwombaji ni mnufaika wa mkopo wa awali ambaye mkopo wake umekwishaiva, anapaswa kuwa amerejesha kiasi chote kilichoiva kinachostahili kurejeshwa.

Mikopo ya Shule ya Sheria itatolewa kugharamia maeneo yafuatayo:

(i) Vitabu na Gharama za Viandikwa;
(ii) Ada ya Mafunzo

13.4 Viwango Vinavyotumika kwa Wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu

13.4.1 Chakula na Malazi

HESLB inatoa mikopo kwa ajili ya chakula na malazi kwa kiasi cha **shilingi 10,000/=** kwa siku wakati wa mafunzo chuoni au wakati wa kukusanya data.

13.4.2 Gharama za Vitabu na Viandikwa

Kiasi cha shilingi 500,000/= kwa mwaka kwa vitabu na viandikwa hutolewa kwa wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu.

13.4.3 Ada ya Mafunzo

HESLB inatoa mikopo ya ada ya mafunzo kwa asilimia mia moja (100%) kulingana na kiwango cha ada cha Taasisi ya Elimu ya Juu husika.

13.4.4 Gharama za Utafiti

HESLB inatoa asilimia mia moja (100%) ya gharama za utafiti kulingana na viwango vinavyotumika na Taasisi ya Elimu ya Juu husika ambavyo huweza kuidhinishwa mara kwa mara.

Viwango vinavyotumika ni kiasi cha shilingi milioni mbili (2,000,000/=) kwa mwaka kwa Shahada ya Uzamili na shilingi milioni tano (5,000,000/=) kwa mwaka kwa Shahada ya Uzamivu.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mtendaji,
BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

17 Julai, 2020